# LEARNING BY EAR.

## Lent Luxury- The risks of raising credit.

## EPISODE NINE: GOOD LOANS & BAD LOANS.

**AUTHOR: James Muhando**

**EDITORS: Adrian Kriesch, Friederike Müller**

**PROOFREADER: Tony Dunham**

**Kisuaheli: Eric Ponda**

**LIST OF CHARACTERS BY SCENE:**

**SCENE ONE: THE FUNDRAISER AT GIDDY'S.**

- **NARRATOR (M 30)**
- **MAMA KELELE(F 65)**
- **WOMAN 1(F 40'S)**
- **YOUNG MAN( M LATE 20'S)**
- **WOMAN 2( F 40'S)**
- **MC (M 40'S)**
- **4 – 5 MIXED CROWD(> 25, GENDER NOT IMPORTANT)**

**SCENE TWO: AT THE MAIZE FIELD.**

- **NARRATOR (M 30)**
- **ZILPAH (F 35)**
- **LUCIA (F NOW 12)**
- **GIDDY (NOW 17)**
- **UNCLE BARRY (40'S)**

**SCENE THREE: BY THE BANKS OF RIVER SABWANI.**

- **GIDDY (M NOW 17)**
- **JENNY (F 15)**

**SCENE FOUR: AT GIDDY'S, UNCLE BARRY CONVINCES ZILPAH.**

- **ZILPAH (F 35)**
- **UNCLE BARRY (M 40)**

**INTRO:**

**1. SFX: OFFICE AMBIENCE. SWIVEL CHAIR**

**2. NARRATOR:**

Hujambo msikilizaji wa makala nyingine ya **Noa Bongo Jenga Maisha Yako**. Leo nakukaribisha katika ofisi yangu mpya tunapoendelea na sehemu ya tisa kwenye mfululizo wa mchezo huu wa redio "**Starehe ya Kuazima- Tatizo la kulipa Mkopo**"! Jina langu ni Gideon Leboo, ofisa wa masuala ya mikopo katiba benki hii ya Jubilee, na pia mhusika mkuu katika mchezo huu. Katika kipindi kilichotangulia, nilikuelezea kuhusu maisha ya ujana wangu, na jinsi mimi na marafiki zangu tulivyojikuta

mashakani kwa sababu ya mkopo. Pia, wazazi wa JD wanazozana baada ya mtoto wao kutoroka nyumbani. Lakini baada ya muda mrefu JD anarejea nyumbani akiwa amebadilika kabisa na kuwa mtu mlevi wa kunywa pombe kupindukia na kuvuta sigara! Muda wote huo, JD alipokuwa ametoroka, tuliendelea na maisha yetu kama kawaida. Mimi na Jenny tulishinda mtihani wetu wa mwisho na kuanza kujiandaa kujiunga na chuo kikuu. Lakini kwa sababu ni watu wa mashambani kutoka jamii maskini wazazi wangu, hawangeweza kugharamia karo ya chuo kikuu. Hivyo, mamangu akaandaa harambee kubwa ya kuchanga pesa kuniwezesha kujiunga na chuo kikuu. Ilikuwa shughuli kubwa iliyogharimu kiasi cha Dola 100 kuandaa chakula na vinywaji. Pia, mama Makelele (Laughs) kama anavyofahamika kutokana na ucheshi wake, alikuwepo!

## SCENE ONE: THE FUNDRAISER AT GIDDY'S

3. **SFX:** **NOISE FROM A CROWD OF PEOPLE, EXTERIOR**

4. **MAMA KELELE: (In a rural accent, loud)** Hawa watoto wamekuwa fahari kubwa kwa kijiji kizima! Ndio watoto wa kwanza kufaulu na kujiunga na "windyvasty"

5. **MEN& WOMEN: BURST OUT LAUGHING.**

6. **WOMAN 1: (Amused)** Chuo kikuu ni “university” Mama Kelele, na sio “windyvasty”!

7. **MAMA KELELE:** Vyovyote vile, mimi sijali? Nachofahamu ni kwamba leo Zilpah anapika kuku kwa sababu ya huyu kijana. Nitakula kushiba leo! Na vijana wengi wanapaswa kujiunga na “Winvasty” ili tuandaliwe karamu mara kwa mara!

8. **MEN&WOMEN: LAUGH.**

9. **YOUNG MAN:** Sikilizeni, Sikilizeni! Hatukuja hapa kwa karamu, tumekuja kuchanga pesa za kumsaidia huyu kijana kujiunga na chuo kikuu kwa masomo zaidi!

10. **MEN&WOMEN: REACT ANNOYED**

***KW begin***

11. **WOMAN 1:** Kaa chini wewe mwanaume! Nani amekupa ruhusa ya kuzungumza kabla ya wazee?

12. **WOMAN 2:** Watoto wa siku hizi hawana heshima kabisa!

13. **MC:** **(Clears his throat )** Sawa ! tusikilizane. Tusikilizane!

14. **CROWD CALMS DOWN GRADUALLY**

15. **MC:** Sote tunafahamu kilichotuleta hapa, sivyo?

16. **CROWD:** Ndio!

17. **MC:** **(Calls)** Tumekuja kufanya nini?

**18. CROWD:** Kuchanga pesa za kumpeleka mtoto wetu chuo kikuu!

**(Mama Kelele is loudest and still says WINDYVASTY!)**

**19. MC:** Sijasikia!

**20. CROWD:** Kumpeleka mtoto wetu chuo kikuu!

***KW End***

**21. MC:** Sawa kabisa! Basi bila kupoteza wakati moja kwa moja tutaanza shughuli hii iliyotuleta hapa! Sasa tupige foleni, kuleta michango yetu kwenye hiki kikapu mmoja baada ya mwengine. Tuko tayari?

**22. CROWD:** Ndio!

**23. MC:** Kwa mara nyingine, tuko tayari?

**24. CROWD:** Ndiooooooooooo!

**25. MC:** Sawa kabisa. Tuanze! Usione haya! Leteni michango yenu!

**26. SFX: CHAIRS AND FOOTSTEPS**

**27. MC:** Mama Eunice dola 4 !

**28. CROWD: APPLAUSES, WOMEN ULULATE.**

**29. MC:** Mzee Harrison dola 10!

**30. CROWD: MORE APPLAUSES.**

**31. MC:** Mama Kelele dola,1! Makofi!

**32. CROWD: NO APPLAUSE, JUST MURMURS.**

**33. MAMA KELELE:(Claps)** Nipigieni makofi! Nipigieni makofi!

**34. CROWD: LAUGHS.**

**35. NARRATOR:**

Wanakijiji wenzangu walichanga na kuchanga, na baada ya shughuli hiyo, tukaandaliwa chakula kilichogharimu dola 100 ,huku tukisubiri hesabu kamili ya pesa zilizochangwa. Kisha kiongozi wa karamu akachukua tena kipaza sauti na kutangaza Dola 70... jumla ya pesa zilizochangwa. Kwetu mimi, na mamangu Lucia lilikuwa pigo kubwa sana, baada ya kutumia dola 100 tumeweza kuchangisha dola 70 pekee, na kupoteza dola 30!

Pengine hutaamini ukisikia ni nani aliyekuja kuokoa jahazi mwishowe! Ni mjombangu Barry! Ndio mwanzo alikuwa ametoka gerezani baada ya kufungwa kutokana na tabia yake ya kujilimbikizia madeni asiyoweza kulipa, na tayari alikuwa ameanzisha kibanda cha kuuza mboga mjini. Biashara ambayo ilikuwa ikifanya vyema sana! Anatukuta shambani mimi na mamangu tukivuna mahindi.

**<u>SCENE TWO: AT THE MAIZE FIELD</u>**

**36. ATMO: MAIZE FIELD, PEOPLE HARVESTING MAIZE**

**37. ZILPAH:** Lucia, mvivu sasa! Nakuangalia tu! Kwanini kila mara wakimbia chooni?

**38. LUCIA:** Tumbo langu linaniuma.

**39. GIDDY:** Huo ni uongo! Wewe ni mvivu tu!

**40. LUCIA:** Funga mdomo wako, Giddy! Wewe ndiye chanzo cha haya yote! Kama isingekuwa ile harambee yako, sisi kama kawaida tungeweza kuwalipa vibarua kufanya hii kazi ya kuondoa mahindi shambani.

**41. ZILPAH:** Nyamaza na uendelee kufanya kazi! Mawingu yameanza kukusanyika na huenda itaanza kunyesha sasa hivi!

**42. SFX:** **FOOTSTEPS ON DRY VEGETATION.**

**43. UNCLE BARRY: (from far)** Habari zenu! Mbona mmekasirika leo?

**44. LUCIA:** **(Happily)** Mjomba Barry!

**45. ZILPAH:** Barnabas! Unafanya nini hapa?

**46. GIDDY:** **(Disinterested)** Habari gani Mjomba!

**47. UNCLE BARRY:** Lucia,kipenzi...! . Giddy!

**48. LUCIA:** Nafurahi sana kukuona mjomba..Lakini Giddy ameanza tena kunichokoza!

**49. UNCLE BARRY:** Usimjali Giddy. Hivi karibuni ataondoka kwenda zake chuo kikuu!

**50. GIDDY:** **(Choked by tears)** Usini.. Usinikumbushe mambo hayo.!

**51. UNCLE BARRY:** Kwa nini? Kuna tatizo gani?

**52. GIDDY:** **(Emotionally)** Mjomba niwache tu!

**53. SFX:** **ANGRY FOOTSTEPS AS GIDDY WALKS AWAY!**

**54. UNCLE BARRY:** Zilpah, huyu kijana anamatatizo gani?. Anaenda wapi?

**55. ZILPAH:** **(Sighs)** Usimjali . Amekasirika kwasababu hataweza kujiunga na chuo kikuu. Twende nyumbani nikakutengenezee kikombe cha chai. Lucia, tafadhali mchunge vizuri haya mahindi, nitarudi sasa hivi!.

**56. SFX:** **FOOTSTEPS ON DRY VEGETATION.**

**57. UNCLE BARRY:** Niambie kuna shida gani?

**58. ZILPAH:** Wewe utafanya nini kutatua shida hiyo hata ukiambiwa? Umetoka gerezani hivi juzi tu, na biashara yako ndio mwanzo inaanza kustawi. .

**59. UNCLE BARRY:** Kwani hujasikia kuhusu mikopo ya kufadhili masomo kutoka halmashauri ya mikopo ya elimu..ehhh?

**60. ZILPAH:** Bado unazungumza kuhusu mikopo, baada ya yote uliyopitia Baranabas.?

61. **UNCLE BARRY:** Kama kuna kitu nimejifunza nikiwa gerezani ni kwamba mikopo yote si hatari!.

62. **ZILPAH:** Tuyaache hayo mambo ya mikopo. Mikopo uliyochukua ndio sababu leo tunajikuta katika balaa hii yote.!!

63. **UNCLE BARRY:** Samahani kwa yote yaliyotokea Dadangu! Lakini tunawajibu wa kumsaidia huyu kijana. Mikopo ya kufadhili masomo si mibaya kwasababu unatumiwa kama ilivyokusudiwa.

64. **ZILPAH:** Na nitapata wapi pesa za kulipa deni hilo.

65. **UNCLE BARRY: (Laughs)** Si wewe utakayelipa mkopo huo!

66. **ZILPAH:** Utalipwa na nani?

67. **UNCLE BARRY:** Giddy!

68. **ZILPAH:** **(Shocked)** Eti nini! vipi?

69. **UNCLE BARRY:** Subiri., Zilpah.nitakuelezea kila kitu tutakapofika nyumbani..

70. **NARRATOR:**

Niliwaacha Mjomba na Familia wakizungumza na mimi ni kashika njia kuelekea mtoni. Niitaka kuwa peke yangu angalau kupunguza hasira na mawazo.. Na kamwe sikutaka kabisa kuwa karibu na mjombangu. Kwani endapo hangeliiba hatimiliki ya shamba letu, pengine mamangu angeliweza kuuza sehemu ya shamba hilo na kunipeleka chuoni. Mtoni

sikutarajia kukutana na mtu yoyote, lakini nilishangaa kumuona Jenny, pia yeye akiwa mwenye mawazo chungu nzima.

**SCENE THREE: BY THE BANKS OF RIVER SABWANI**

**71. ATMO: RIVER FLOWING**

**72. SFX: FOOTSTEPS**

**73. GIDDY:** Jenny? Kumbe uko hapa?. Tunaweza kukaa pamoja.?

**74. JENNY:** Sawa!.

**75. GIDDY:** Unafanya nini peke yako hapa?

**76. JENNY:** **(Sighs)** Nina waza tu..

**77. GIDDY:** Unawaza nini..?

**78. JENNY:** Kuhusu maisha!, Chuo kikuu na jinsi mambo yanavyokwenda na kwamba huenda sitaweza kujiunga na chuo kwa sababu ya kukosa karo.

**79. GIDDY:** **(Sighs)** Ni kweli. Hata mimi pia!

**80. JENNY:** Sasa kuna haja gani?

**81. GIDDY:** Kwanini…? haja ya nini?

**82. JENNY:** Kuna haja gani ya kupoteza miaka 12 ukisoma katika shule ya msingi na kufauli ,kisha unaishia tu kama mtu ambaye hakwenda shule kabisa?

**83. GIDDY:** **(Soothingly)** Jenny. Usijilaumu. Si makosa yako. Isitoshe, familia yako, kama ilivyo yangu, haina uwezo huo.

**84. JENNY:** Lakini Giddy, nafikiri wazazi wetu wangeweza kufanya vyema zaidi kuliko sasa.

**85. GIDDY:** Vipi?

**86. JENNY:** Kwa kuweka akiba zaidi na kubana matumizi! Mara nyingine nilikuwa nikimuona mamangu akinunua vitu ambavyo havina umuhimu sana. Mfano viatu ambavyo mara nyingi alikuwa havivai!

***KW begin***

**87. GIDDY:** Jenny, kwa nini mamako asichukue mkopo wa benki?

**88. JENNY:** Mkopo wa benki? Ulimsikia Bw. Mando alivyosema? Lazima uwe na dhamana ili kupata mkopo huo wa benki. Mamangu hana kazi wala chochote anachoweza kutumia kama dhamana!

**89. GIDDY:** Na je shamba lenu? Kwani hilo si mali?

**90. JENNY:** **(Shocked)** Nini ! Ni watu wangapi wamepoteza mali zao kupitia njia hiyo? Huwezi kucheza kamari na tegemeo letu la pekee maishani, eti kwa sababu ya dhamana ya mkopo! Na je, tukishindwa kulipa mkopo huo?

***KW end***

**91. GIDDY:** Nimekuelewa sasa!. Lakini usikate tama!. Bado tuna wiki mbili kabla muda huo wa kijiunga na chuo kumalizika.!

**92. SFX: THUNDER**

**93. GIDDY:** Twende nyumbani sasa, naona mvua itaanza kunyesha!

**<u>SCENE FOUR:AT GIDDY'S.</u>**

**94. SFX: TEA POURED INTO TIN CUPS.**

**95. ZILPAH:** Chai iko tayari kakangu!. Hata kama tumeshindwa kumpeleka mtoto wetu chuo kikuu, hatuwezi kushindwa na kikombe cha chai.

**96. UNCLE BARRY:** Nakwambia, Zilpah! Bado hatujachelewa! Naweza kukupeleka kwa Bw. Mando anafanya kazi katika benki na nina uhakika ataweza kutusadia kupata mkopo.

**97. ZILPAH:** **(Unsure)** Barnabas,mimi sidhan! Kwani unamfahamu yoyote aliyenufaika kutokana na mpango huu wa Mkopo wa masomo kwa wanafunzi.?

**98. UNCLE BARRY** Yeye mwenyewe Bw. Mando kwanza!

**99. ZILPAH:** Lakini mkopo huu unafanya kazi vipi?

**100. UNCLE BARRY:** Mkopo huu ni mpango wa serikali ambao unakusudiwa kuwasaidia watoto werevu kutoka jamaa maskini kugharamia masomo yao. Hutolewa kwa wanafunzi ambao kwa hakika hawawezi kulipa karo..

**101. ZILPAH:** Lakini bado huo ni Mkopo tu,! na lazima wakati mmoja utahitajika kuulipa na pengine sitaweza. Isitoshe sina dhamana ya kuchukua mkopo huo.

**102. UNCLE BARRY:** Sikiliza, huu mkopo hauhitaji dhamana yoyote! Giddy ataulipa, na kwa hakika anasta hili kupewa mkopo huu kupitia mpango wa *deferment*.

**103. ZILPAH:** Na ni nini hiyo? eti *Def*...nini?

**104. UNCLE BARRY:** *Deferment*. Ni malipo ya mkopo huo ambayo huahirishwa hadi pale mwanafunzi atakuwa tu na uwezo wa kuanza kuulipa.Mfano wakati anapoajiriwa, au akianzisha biashara.. Katika mataifa mengi duniani, wanafunzi wengi wamenufaika sana na mpango huu.

**105. ZILPAH:** Na kwanini mkopo huu ni mzuri kuliko ile uliyokuwa ukichukua? Na unahakika gani kwamba sitahangaishwa kama ulivyohangaishwa wewe?

**106. UNCLE BARRY:** Nilifanya makosa!. Kwanza kabisa sikuwa na malengo ya moja kwa moja kuhusu miradi niliyotaka kutekeleza kupitia mkopo huu. Nilichukua mkopo bila

ya sababu zozote. Lakini mkopo huu wa elimu ninaweza kusema ni mkopo mzuri kwa sababu unalipwa moja kwa moja kwa taasisi au chuo cha mafunzo, na hivyo kutumiwa kwa malengo yanayokusudiwa.

**107. SFX:** **THUNDER AS IT STARTS TO RAIN.**

**108. ZILPAH:** **(Urgently)** Fanya upesi! Njoo tukamsaidie Lucia kuondoa mahindi shambani kabla mvua haijaanza kunyesha!

**OUTRO :**

**109. SFX:** **OFFICE ATMO**

**110. NARRATOR:**

Je unaweza kuamini uliyosikia?. Kutokana na ushauri wa Mjomba Barry hatimaye tunafaulu kujiunga na chuo kikuu! Amini usiamini, yote yalitokana na mkopo uliotuwezesha mimi na Jenny kupata nafasi ya kuendelea na masomo yetu chuo kikuu! Na ndio maana sasa nafanya kazi katika benki hii. Kwa hiyo, sio mikopo yote ni mibaya! Mfano mkopo wa kufadhili masomo ni mzuri sana kwa sababu unawapa nafasi wanafunzi werevu kutoka jamii maskini kuendelea na masomo yao (Sighs)

Muda wangu umekwisha na sasa nitarudi kuendelea na kazi. Lakini katika kipindi kinachofuata nitatembelea jamaa na marafiki kijijini

kuwajulia hali. Kwa hiyo, ukitaka kusikia mengi zaidi kuhusu mjomba Barry na marafiki wangu wote wanavyoendelea usikose kujiunga nami wakati huo. Ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtandao wetu wa dw.de/lbe. Hadi wakati mwengine kwaheri kwa sasa!